



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatarajia kuendesha Uchaguzi wa Mbunge wa Jimbo la Amani kwa upande wa Unguja - Tanzania Zanzibar, Disemba 2022. Katika kutekeleza jukumu hilo, Tume inatangaza nafasi za kazi za muda ili kupata Watendaji watakaosimamia zoezi hilo. Nafasi za kazi hizo ni kama zifuatazo: -

1. Msimamizi wa Uchaguzi (*Nafasi moja*)

Majukumu

- (i) Kuratibu na kusimamia shughuli za Uchaguzi katika Wilaya yake.
- (ii) Kusimamia na kufuatilia utendaji kazi wa Watendaji wa Uchaguzi walio chini yake.
- (iii) Kutunza vifaa vya Uchaguzi katika Wilaya husika.
- (iv) Kusimamia matumizi ya fedha za Uchaguzi.
- (v) Kushirikiana na kushauriana na Mratibu wa Uchaguzi katika kuleta ufanisi kwenye shughuli za Uchaguzi.
- (vi) Kutoa taarifa ya mwenendo wa hatua za uchaguzi kwa kuzingatia maelekezo ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi.

Sifa za Msimamizi wa Uchaguzi

- (i) Awe raia wa Tanzania.
- (ii) Awe mtumishi wa Umma.
- (iii) Awe na Shahada au stashahada ya juu au Stashahada katika fani yoyote.
- (iv) Awe mkazi wa Wilaya husika.
- (v) Awe muadilifu na mwaminifu.

- (vi) Awe tayari kujituma na kuweza kufanya kazi bila ya usimamizi wa karibu.
- (vii) Awe na uzoefu katika masuala ya Uchaguzi/Uandikishaji wa Wapiga Kura.

2. Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi Ngazi ya Jimbo (Nafasi mbili)

Majukumu

- (i) Kuwa kiungo kati ya Jimbo na Wilaya.
- (ii) Kusimamia shughuli zote za Uchaguzi katika Jimbo husika.
- (iii) Kumsaidia Msimamizi wa Uchaguzi katika masuala yote ya Uchaguzi.

Sifa za Mwombaji

- (i) Awe raia wa Tanzania.
- (ii) Awe ni Mtumishi wa Umma.
- (iii) Awe na Shahada au Stashahada ya juu au stashahada katika fani yoyote.
- (iv) Awe mkazi wa Wilaya husika.
- (v) Awe tayari kujituma na kuweza kufanya kazi bila ya usimamizi wa karibu.
- (vi) Awe na Uzoefu katika masuala ya Uchaguzi/Uandikishaji wa Wapiga Kura.
- (vii) Awe muadilifu na mwaminifu.

Kila Mwombaji katika nafasi husika aainishe nafasi anayoiomba na aambatishe maelezo ya taarifa binafsi (CV) akiweka Jina la Taasisi anayofanyia kazi na cheo chake. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 10 Novemba, 2022.

Barua zote zielekezwe kwa:

Mkurugenzi wa Uchaguzi,
Tume ya Taifa ya Uchaguzi,
Ofisi ya Zanzibar,
Mtaa wa Maisara,
S. L. P. 4670,
Zanzibar.

NB: Kwa urahisi maombi yote yatapokelewa

Unguja – Ofisi ya NEC – Maisara, Unguja.